

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّكُمْ وَعَمِلْتُمُ الصَّالِحَاتِ لَتُسْتَخْفَفُوهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْفَفْتُمُ الْأَيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُخْكِنَنَّكُمْ دِيْنُكُمْ إِنَّمَا أَنْهَاكُمْ عَنِ الْأَرْضِ مَمْ لَيُكَلِّمُنَّكُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقَتِهِمْ أَمْنًا يَعْدُونَنِي لَا يُشْكُرُونَ فِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّاغِنُونَ



Na: 1445 H / 038

Jumatano, 7 Dhu al-Qa'adah 1445 H

15/05/2024 M

Taarifa kwa Vyombo vya Habari**Gaza ina Vifusi Vingi kuliko Ukraine, na Dada zetu na Watoto Wetu ndio Wengi wa Wafu Wanaozikwa Chini Yake (Imetafsiriwa)**

Shirika la Wanawake la UN lilitoa ripoti mnamo mwezi Aprili 2024, kuhusu hali ya wanawake na watoto mjini Gaza. Miezi sita ya vita hivyo, zaidi ya wanawake 10,000 wameuawa, kati yao kina mama wanaokadiriwa kufikia 6,000, na kuacha watoto 19,000 wakiwa yatima. Al Jazeera inakadiria kuwa wanawake na watoto 25,000 wameuawa. Huku zaidi ya waandishi huru wa habari 100 kuuawa na bila ya kuwepo jopo liliopangiliwa la wachunguzi kuruhusiwa kuwepo katika eneo hilo, ni vigumu sana kufuatilia idadi kamili, na ni lazima tuchukulie kwamba takwimu hizi ziko chini ya uhalisia.

Mnamo tarehe 2 Mei 2024, Charles Mungo Birch, mkuu wa Huduma ya Utekelezaji Migodi ya Umoja wa Mataifa @UNMAS nchini Palestina alitoa taarifa ya umma duniani kote. Katika taarifa yake rasmi kwa vyombo vya habari yafuatayo yalielezwa: "Gaza ina vifusi vingi zaidi kuliko Ukraine, na ili kuweka hilo katika mtazamo, mstari wa mbele wa Ukraine una urefu wa maili 600, na Gaza ni maili 25." Aliongeza kuwa kuna zaidi ya tani milioni 37 za uchafu wa kuondolewa huko Gaza mara tu vita vya "Israel" kwenye Ukanda huo vitakapomalizika.

Kiwango cha ulipuaji wa mabomu na maangamizi hakijawahi kutokea katika historia ya ulimwengu, kwa muungano wa wasaidizi waovu wa mauaji yanayopatikana katika serikali fisadi za kikoloni za Magharibi na watumwa wao kwa sura ya watawala wote katika ardhi zetu za Kiislamu. Tunachopaswa kutambua katika kuangalia idadi kubwa ya vifo vya wanawake na watoto ni kwamba maelfu ya wanawake na watoto waliorodheshwa wamekuwa wanasalia chini ya vifusi anavyozungumzia. Wengi walikufa papo hapo huku wengi wakifa polepole na vifo vya uchungu kwa siku nyingi wakisubiri kuokolewa bila mtu wa kuwaokoa. Wafanyakazi wa misaada na majirani, pamoja na wanafamilia, wameripoti kuwa waliweza kusikia mayowe ya watoto na wengine wakiwa hai, lakini kutokana na ukosefu wa vifaa au mafuta ya kuwakisha mitambo ya uokozi, iliwalazimu kuwaacha wakiwa wamenaswa na hatima yao isiyoepukika.

Hata kazi ya kuwatoa wafu, katika hali yoyote ya kupata mwili, imekabiliwa na changamoto kubwa. Mungo alielea kuwa kifusi hicho kimechafuliwa kwa kiasi kikubwa na UXO (Unexploded Ordnance) pamoja na kemikali zinazotumika katika vita. Aliongeza kuwa zaidi ya tani 800,000 za asbesto pia ni hatari halisi na iliyoko.

Je, mipango ya uvezeshaji wanawake inaweza kuchukuliwa kwa uzito tena!? Watetezi wa haki za wanawake na sheria za kimataifa juu ya uvezeshaji wanawake, unyanyasaji dhidi ya wanawake na haki za wanawake wote wamethibitika kuwa uongo mtupu, na sheria hizi zinatumika tu kushambulia sheria za Kiislamu na kudhibiti kuenea kwa Uislamu. Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa lilizindua Tahadhari ya hivi punde ya Jinsia kuhusu Gaza miezi sita tangu vita, na inakadiria kuwa kina mama 6,000 wameuawa, na kuwaacha watoto 19,000 wakiwa yatima. Wanawake ambao wamenusurika katika mashambulizi ya mabomu na operesheni za ardini za umbile la Kiyahudi wamehamishwa, ni wajane, vilema na wanakabiliwa na njaa. Hakika hivi ni vita dhidi ya wanawake na watoto.

Kwa mwanamke yejote wa Kiislamu ambaye anaendelea kuwa na imani au matumaini katika mifumo, sheria na taasisi za kisekula ili kuwaokoa dada zao Waislamu huko Gaza au kwengineko kutokana na mauaji na maangamizi, hakika sasa ni wakati wa kuzika matumaini yako katika vifusi na magofu ya demokrasia ya Magharibi, na badala yake waungane katika ulinganizi wa kusimamishwa kwa haraka Mfumo wa Mwenyezi Mungu (swt), Khilafah kwa njia ya Utume ambayo itamuondo kila mtawala kibaraka katika ardhi zetu na kuyakusanya majeshi ya Kiislamu kutimiza wajibu wao kwa Mwenyezi Mungu wa kuwalinda, kuwatetea na kuwakomboa Waislamu.

[وَمَنْ يُؤْلَمُ بِمَنْ دَبَرَ إِلَّا مُتَحَرِّفٌ لِّقَاتَالِ إِلَى فِتْنَةٍ فَقَدْ بَاءَ بِعَذَابٍ مِّنَ اللَّهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ]

"Na atakaye wageuzia mgongo wake siku hiyo - isipo kuwa kwa mbinu za vita au kuungana na kikosi - basi atakuwa amestahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na pahala pake ni Jahannamu, na huo ni mwisho muovu." [Al-Anfal: 16]

Kitengo cha Wanawake
katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

